**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

# MWONGOZO WA KUOGESHA MIFUGO



**IMETOLEWA NA KATIBU MKUU MIFUGO**

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

**OKTOBA 2019**

## 1.0 UTANGULIZI

Magonjwa yaenezwayo na kupe hususan Ndigana Kali (ECF) ni miongoni mwa changamoto kubwa katika maendeleo ya Sekta ya Mifugo kwa kuwa yanasababisha vifo vingi vya ng'ombe. Magonjwa yaenezwayo na kupe hudhibitiwa kwa kutumia njia mbalimbali ambapo njia kuu ni matumizi ya dawa za kuua kupe (viuatilifu vya mifugo) kwa kuogesha au kunyunyiza mifugo. Njia zingine ni kutoa chanjo dhidi ya Ndigana Kali na matibabu.

Ikumbukwe kuwa hapo zamani uogeshaji ulikuwa unagharamiwa na Serikali na wafugaji walikuwa wanaogesha bure. Kutokana na ufinyu wa bajeti na mabadiliko ya sera gharama za uogeshaji zilibaki mikononi mwa wafugaji wenyewe na matokeo yake wafugaji wengi walikosa mwamko wa kuogesha mifugo. Kutokana na kukosa mwamko wa uogeshaji mifugo dhidi ya kupe; magonjwa yaenezwayo na kupe yamekithiri nchi nzima na yamekuwa yanasababisha hasara kubwa kutokana na vifo vya wanyama. Kwa mujibu wa taarifa zilizopo, magonjwa yaenezwayo na kupe huchangia asilimia **72** ya vifo vyote vya mifugo hususan ng'ombe. Magonjwa hayo na asilimia ya uchangiaji kwenye vifo ni Ndigana Kali (**43.7**), Ndigana Baridi (**16.6)**, Maji Moyo (**6.5)** na Mkojo mwekundu (**5.2)**. Hii yote imechangiwa sana na uhaba wa majosho, na majosho yaliyopo mengi hayatumiki kwa sababu ya kuharibika na pia uangalizi hafifu.

Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imekua ikinunua dawa za kuogesha mifugo kwa lengo la kuhamasisha wafugaji kuogesha mifugo yao na hivyo kuwa na ufugaji wenye tija. Dawa zinazonunuliwa zinaelekezwa kwenye majosho mazima yanayofanya kazi ama yenye uwezo wa kufanyakazi. Dawa za kuogesha zinanunuliwa aina tofauti kulingana na uwezo wa dawa hiyo kuuwa kupe na wadudu wengine katika eneo husika na pia kutokana na ushauri au maelekezo ya Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo Nchini.

Awamu ya kwanza ya kuogesha mifugo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilinunua dawa za kuogesha lita **8,823.56** aina ya Paranex zenye thamani ya shilingi **300,000,000** ambazo ziligawanywa katika majosho **1,486** katika Mikoa **25** Nchini. Jumla ya michovyo iliyofanyika ni ya mifugo **43,566,163** wakiwemo ng'ombe **26,366,735**, mbuzi **12,534,683**, Kondoo **4,434,163**, punda **1,755** na mbwa **229,326**. Aidha vikundi **847** vilianzishwa na kati ya hivyo **612** vilifungua akaunti.

Katika awamu ya pili ya uogeshaji mifugo Wizara ya mifugo na Uvuvi imenunua dawa ya kuogesha mifugo lita **12,549.50** (Paranex lita **11,484.50** na Amitraz lita **1,065**) zenye thamani ya Sh **440, 714,750.00** ambazo zitasambazwa katika Mikoa 25 Tanzania Bara. Aidha dawa hizi zitagawiwa kwenye **1,738** ambayo ni ongezeko la majosho **252** kati ya hayo **247** yamekarabatiwa na **5** mapya yamejengwa. Zoezi hili litahusisha mifugo aina ya ng'ombe, mbuzi, kondoo na punda. Mchanganuo wa mgao wa dawa za kuogesha mifugo kwa kila wilaya umeoneshwa katika kiamba Na 1. Vivyo hivyo majosho mapya yatayojengwa na yale yatakayokarabatiwa yatapatiwa dawa na Wizara.

Ili kufanikisha kikamilifu zoezi la uogeshaji mifugo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeandaa Mwongozo na Kanuni za usimamizi wa dawa za kuogesha mifugo na uogeshaji za

mwaka 2019 wa Kuogesha Mifugo ambazo zimeainisha utaratibu na majukumu yatakayofuatwa kuanzia Serikali kuu mpaka Serikali za Mitaa kwa lengo la kuwa na uogeshaji endelevu. Aidha, katika sehemu ya III ya Kanuni hii kifungu cha 20 (1) na (2) kimeeleza kuwa jukumu la uogeshaji mifugo ni la lazima kwa wafugaji wote.

Mwongozo huu unasimamiwa na Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Namba 17 ya Mwaka 2003 na Kanuni za Uogeshaji mifugo za Mwaka 2019. Aidha, usambazaji wa dawa kwa ajili ya awamu ya pili ya kuogesha mifugo utaanza tarehe 19/10/2019 na uogeshaji wa mifugo kwa kutumia dawa hizo utaanza rasmi tarehe **01/11/2019** kwa nchi nzima.

## 2.0 MAJUKUMU YA WADAU:

### 2.1 Wizara na Vituo vya Huduma za Mifugo vya Kanda

Katika kanuni sehemu ya III vifungu vya 26 na 27 vimeelezea majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na majukumu ya kimaabara katika kuhakikisha dawa inayotumika ina ubora unaostahili.

- 2.1.1 Kuunda timu za kikanda za uhamasishaji, ufuatiliaji na majukumu yake kiambatisho Na 2.
- 2.1.2 Kujiridhisha/kuhakiki ikiwa majosho yanafanyakazi, mifugo inaogeshwa, usimamizi na ukusanyaji wa fedha za uogeshaji, vikundi kama vipo na vinafanyakazi na kama vimesajiriwa
- 2.1.3 Kushirikiana na uongozi wa vijiji/kata, chama cha wafugaji na maafisa maendeleo ya jamii kuhamasisha uundaji wa vikundi vya majosho mahali ambapo havipo na kuviwezesha kusajiriwa.
- 2.1.4 ZVC kupima mara kwa mara ubora na uwezo wa dawa kufanyakazi kwa kushirikiana kamati ya majosho, TVLA na Wizara kwa ujumla.

### 2.2 Majukumu ya Timu za kikanda za Uhamasishaji na Ufuatiliaji:

- 2.2.1 Uhamasishaji wa matumizi sahihi ya dawa, uogeshaji na matumizi bora ya josho
- 2.2.2 Usimamizi wa usambazaji wa dawa ya josho kutoka ngazi ya Mkoa hadi kwenye kijiji (majosho)
- 2.2.3 Kufuatilia majosho yaliyoainishwa kama yapo na yanatoa huduma.
- 2.2.4 Usajili na utendaji kazi wa kamati au vikundi vinavyoendesha majosho
- 2.2.5 Ufuatiliaji wa zoezi la uogeshaji mifugo kwenye majosho.
- 2.2.6 Ufuatiliaji wa utaratibu wa ukusanyaji mapato ya kuogesha na urejeshaji wa fedha kwa mzabuni wa dawa ya josho kwa lengo la kununua dawa nyingine.
- 2.2.7 Kufuatilia utaratibu wa kuweka kumbukumbu za uogeshaji na ukusanyaji mapato.
- 2.2.8 Kutoa ushauri katika ngazi zote za ufuatiliaji na kufanya marekebisho pale inapobidi.
- 2.2.9 Kufanya vikao katika ngazi mbalimbali za ufuatiliaji.
- 2.2.10 Kuandika taarifa mbalimbali za ufuatiliaji na utekelezaji wa kazi hizo.

### 2.3 Majukumu ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa

2.3.1 Kupokea dawa ya kuogesha mifugo toka kwa mzabuni au msambazaji kwa kufuata taratibu za stoo ikiwa ni pamoja na matumizi ya; ***receipt voucher***, ***ledger*** na ***delivery note***.
2.3.2 Kuhifadhi dawa za kuogesha mifugo kwa muda kabla hazijasambazwa Wilayani.
2.3.3 Kutoa maelekezo kwa Halmashauri za Wilaya kuhusu kiasi cha dawa za kuogesha mifugo walizopangiwa na kuwakabidhi.
2.3.4 Kushirikiana na timu ya Wizara ya mifugo kufuatilia zoezi la usambazaji na matumizi ya dawa hizo kulingana na maelekezo yaliyotolewa na Wizara.
2.3.5 Kuhamasisha ngazi ya Halmashauri juu ya uogeshaji wa mifugo

## 2.4 Majukumu ya Halmashauri za Wilaya/Manispaa/Miji

Halmashauri kuandaa utaratibu mzuri wa kuendesha na kusimamia majosho yote yatakayopewa dawa. Sehemu ya III ya Kanuni ya uogeshaji mifugo kifungu cha 21 (1) hadi (8) kimeelezea majukumu ya Serikali za Mitaa/Halmashauri pamoja na majukumu mengine kama yalivyoelekezwa na mwongozo kama ifuatavyo:

2.4.1 Kugawa dawa kwa kila josho kwa kuzingatia taratibu za stoo.
2.4.2 Kuwezesha josho kuendeshwa na kikundi kwa makubaliano sahihi Kikundi au kamati ya joshoiwe inatokana na watumiaji wa josho
2.4.3 Kuandaa ratiba za uogeshaji kwa kushirikiana na uongozi wa majosho na Serikali za Vijiji husika.
2.4.4 Kuhakikisha kila josho linakuwa na uongozi
2.4.5 Kusimamia uendeshaji wa majosho na kuhakikisha uongozi wa josho unatoa taarifa ya uogeshaji kwenye Serikali ya kijiji na kwa Daktari wa Mifugo wa Wilaya.
2.4.6 Kuhakikisha kila josho linakuwa na akaunti yake Benki.
2.4.7 Kusimamia kila kikundi /Kamati kuwa na mfumo mzuri wa ukusanyaji wa mapato na matumizi mazuri ya mapato hayo.
2.4.8 Kusimamia upatikanaji wa mhudumu wa josho (dip attendant) na kufanikisha mafunzo mafupi kwa wahudumu wa majosho (dip attendant) kuhusu uendeshaji wa josho
2.4.9 Kushirikiana na kikundi/kamati ya josho kuhakikisha uwepo wa mfumo endelevu wa upatikanaji wa dawa
2.4.10 Kuweka taratibu za kuweka fedha kwenye akaunti za benki za vikundi vya uogeshaji na baadaye kununua dawa nyingine za kuogesha (acaricides)
2.4.11 Kuratibu na kusimamia uwekaji mzuri wa kumbukumbu, kuandaa tarifa za uogeshaji na kuzituma Zonal Veterinary Center (ZVC) na Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa
2.4.12 Kukarabati na kujenga majosho mapya kulingana na mahitaji ya wafugaji kama ilivyoainishwa kwenye Waraka wa Rais na. 1 wa mwaka 2002 "Kuhusu Kuzuia Kuenea kwa Magonjwa ya Mifugo Nchini", kipengele cha 6: "Uogeshaji wa Mifugo na Uzuiaji *wa Kupe na Magonjwa ya Kupe"*

## 2.5 Serikali za Vijiji/Kata

Katika kifungu cha 28,29 na 30 cha Kanuni ya uogeshaji mifugo imeelekeza majukumu ya viongozi mbalimbali wakiwemo viongozi wa jadi, wafugaji, vyama vya wafugaji na Maafisa Mifugo

2.5.1 Kuhamasisha wafugaji kuogesha mifugo yao kwa kuzingatia ratiba itakayotolewa
2.5.2 Kusimamia uogeshaji kwa kutumia Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Na 17 ya Mwaka 2003 na kanuni za uogeshaji mifugo za mwaka 2019 ambazo zinamtaka kila mfugaji kuogesha mifugo yake na kuwachukulia hatua wasiotekeleza kulingana na adhabu zilizopo kwenye kanuni za uogeshaji.
2.5.3 Kupokea na kutathmini taarifa ya uendeshaji wa josho kulingana na kanuni za katiba ya kikundi/kamati.

### 2.6 Kikundi/Kamati ya uendeshaji majosho

Katika sehemu ya II ya Kanuni ya uogeshaji Mifugo kifungu cha 13 (1) na (2) kimeeleza majukumu ya kamati ya uendeshaji wa josho na sehemu ya III kifungu cha 24 na 25 kimeelezea utoaji wa taarifa na kufungua akaunti ya josho na uendeshaji wake.

2.6.1 Kuhamasisha wafugaji na kuhimiza uogeshaji endelevu.
2.6.2 Kuweka ratiba na utaratibu wa kuendesha na kusimamia uogeshaji
2.6.3 Kamati itakusanya fedha zitokanazo na uogeshaji na kuziweka benki kwenye akaunti ya kikundi.
2.6.4 Kupanga matumizi katika kununua dawa ya kujazia (replenishment), kulipa mhudumu wa josho, kuweka maji na usafi wa josho.
2.6.5 Kikundi/kamati itanunua dawa ya josho kwa kupata ushauri toka kwa Daktari wa Mifugo wa Wilaya au Afisa Mifugo/Ugani husika. Kusimamia ujazaji wa maji na uongezaji dawa kwenye majosho (replenishment) kutokana na ushauri na maelekezo ya Afisa Mifugo/Ugani.
2.6.6 Kununua dawa za kujazia (replenshment) kutoka kwa mzabuni aliyeteuliwa na serikali
2.6.7 Kufanya matengenezo madogo kwenye josho ambayo hayahitaji ushauri wa kitaalamu toka kwa Mhandisi.
2.6.8 Afisa Mifugo/Ugani atakuwa msimamizi wa josho na kutoa ushauri wa Kitaalamu kwa kamati/kikundi kinachosimamia josho.
2.6.9 Kutoa tarifa ya fedha na uogeshaji kwenye serikali ya kijiji
2.6.10 Kuhakikisha kwamba baada ya wafugaji hawachangishwi fedha yoyote ndani ya miezi sita baada ya kulipia shilingi 600 kwa ng’ombe na shilingi 120 kwa Mbuzi/kondoo.

### 2.7 Majukumu ya mfugaji

2.7.1 Kuwajibika kuogesha mifugo yake katika josho kulingana Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Na 17 ya Mwaka 2003 na kanuni zake pamoja na ratiba iliyowekwa na kamati ya josho.
2.7.2 Kuchangia gharama ya kuogeshea mifugo shilingi 600 kwa ng’ombe na shilingi 120 kwa Mbuzi/kondoo gharama inayotosheleza kuogesha kwa muda wa miezi 6 au kulingana na michovyo itakavyohitaji.

## 3.0 MAKADIRIO YA MALIPO NA MAKUSANYO YA UOGESHAJI

### 3.1 Gharama ya Uogeshaji kwa Mfugaji kwa Muda wa Miezi sita ya Mwanzo

Kifungu cha 23 (1) hadi (3) cha Kanuni kimetoa maelekezo juu ya upangaji wa bei za kuogeshea mifugo kwa aina ya dawa inayotumika.

3.1.1 Mfugaji ataogesha mifugo yake kwa muda wa miezi sita (6) mfululizo kwa kuchangia gharama ya shilingi 600 kwa kila ng'ombe mmoja na shilingi 120 kwa kila mbuzi na kondoo kwa miezi sita.

3.1.2 Katika muda wa miezi sita wa uogeshaji, fedha iliyochangwa na wafugaji itatumika katika kununua dawa ya kuongeza kwenye josho (replenishment), kujaza maji na kulipa muhudumu wa josho.

## 3.2 Ufafanuzi wa Gharama za Uogeshaji

3.2.1 Ni matumaini ya Wizara kuwa Shilingi 600 kwa ng'ombe na 120 kwa mbuzi/kondoo zitatolewa mara moja, Aidha kwa kipindi cha miezi 6 wafugaji hawatachangishwa kiasi chochote cha fedha kwa ajili ya shughuli za uogeshaji kwa dawa hizi za ruzuku.